

Uenezi na Changamoto za Kiswahili Nchini Burundi

Enock Havyarimana

Advanced School of Translators and Interpreters (ASTI), Pan African University (PAU), Cameroon.
enochelle1@gmail.com

Correspondence: enochelle1@gmail.com

Received: November 06, 2023; **Accepted:** December 05, 2023; **Published:** 29 December 29, 2023

Abstract: Despite being the second most spoken foreign language in Burundi, Kiswahili is still given little attention compared to French and English. This study therefore aimed to investigate the spread of Kiswahili in Burundi by highlighting the challenges and factors that led to its spread in the country. Primary and secondary data were used in this study where primary data were collected through interviews. In addition, a population of 41 respondents was made up of Kiswahili teachers at universities and residents of the provinces of Rumonge, Makamba, Muyinga and the economic city of Bujumbura. This study which was conducted in Burundi revealed that Kiswahili spread in Burundi thanks to religion, immigration, the arrival of Arabs, colonialism, regional cooperation, war, business, education, marriage, border interactions and media. Although Kiswahili is taught from primary school to universities and the presence of associations to promote it, this study revealed that the history of Burundi, shortage of teachers and books, misconceptions, language policy and social classes are among the challenges that hinder the rapid development of the language. This study concluded by recommending the wide use of the language in different sectors and carrying out researches on the current status of Kiswahili in Burundi.

Keywords: Burundi, Challenges, East Africa, Kiswahili, Spread

IKISIRI: Licha ya umaarufu wa kuwa lugha ya pili ya kigeni inayozungumzwa sana nchini Burundi, Kiswahili bado kinapewa nafasi ndogo sana ikilinganishwa na Kifaransa na Kiingereza. Hivyo, utafiti huu ulilenga kuchunguza hali ya Kiswahili nchini Burundi kwa kuangazia changamoto na sababu zilizopelekea kusambaa kwa lugha hiyo ya kigeni nchini humo. Data za uwandani na data za marejeleo zilitumika katika utafiti huu ambapo data za uwandani zilikusanywa kwa njia ya usaili. Aidha, sampuli ya watafitiwa 41 iliundwa na walimu wa Kiswahili vyuo vikuu na wenyeji wa mikoa ya Rumonge, Makamba, Muyinga na jiji la Bujumbura. Utafiti huu ambao ulifanyika nchini Burundi ulibaini kuwa Kiswahili kilisambaa Burundi kutokana na dini, uhamiaji, ujio wa Waarabu, ukoloni, ushirikiano wa kikanda, vita, biashara, elimu, ndoa, maingiliano ya mpakani na vyombo vya habari. Licha ya Kiswahili kufundishwa kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo vikuu na uwepo wa vyama vya kukiendeleza, utafiti huu ulibaini kuwa historia ya Burundi, uhaba wa walimu na vitabu, mitazamo potofu, sera ya lugha na matabaka ya kiuchumi ni miongoni mwa changamoto zinazotatiza maendeleo ya lugha hiyo. Utafiti huu unahitimisha kwa kupendekeza matumizi mapana ya lugha hiyo katika nyanja zote na kufanya utafiti wa kina kuhusu mafanikio ya Kiswahili nchini Burundi.

Maneno ya msingi: Afrika Mashariki, Burundi, Changamoto, Kiswahili, Uenezi

1. Utangulizi

Kama tunavyojua tayari lugha ya Kiswahili imeenea katika mataifa mbalimbali duniani licha ya chimbuko lake kuwa pwani ya Afrika Mashariki (Kakama, 2019: 15; Choge, 2020: 1). Kwa mujibu wa Kandagor (2018: 32), akiungwa mkono na Mohamed (1993: 9)

Kiswahili ni mojawapo ya lugha za Kibantu inayozungumzwa katika mataifa mengi ulimwenguni, hasa katika ukanda wa Afrika Mashariki. Katika ngazi za kimataifa, mataifa ya Kimagharibi na Mashariki hutumia Kiswahili kwa kiwango kikubwa, kwa mfano katika taasisi za elimu, vyombo vya habari na miktadha mingine kama vile biashara na utalii.

Njia mbalimbali zilitumika katika kusambaza lugha hiyo nje ya mipaka yake ya asili. Habwe (2021) anajadili baadhi ya sababu zilizopelekea kuenea kwa Kiswahili nchini Sudan Kusini. Sababu hizo ni biashara, elimu, uhamiaji, dini, vita na mitagusano ya mpakani. Choge (2020: 3) anaeleza sababu za kuenea kwa Kiswahili: elimu, biashara, nafasi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, vyombo vya habari, mikakati ya kukuza utaifa, mwamko wa uanaafrika uliolenga kubuniwa kwa taifa moja la Afrika. Naye Ababaker (2013) anadai kuwa lugha ya Kiswahili imeathiriwa pakubwa na shughuli mbalimbali za Waarabu kama vile: dini, biashara, siasa na utawala.

Lugha ya Kiswahili inaendelea kukua kwa kasi kubwa sana. Kwa mujibu wa Lianza (2021), “Kiswahili ni miongoni mwa lugha kumi maarufu duniani, na yenye wazungumzaji wapatao milioni 200 kulingana na ripoti ya shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).” Mtafiti huyo anaendelea kudai kuwa Kiswahili kinazungumzwa katika nchi 14 kama vile: Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudan Kusini, Somalia, Msumbiji, Malawi, Zambia, Visiwa vya Komoro, vilevile nchini Oman na Yemen ukanda wa Mashariki ya Katika.

Habwe (2021) anadokeza kuwa nchini Uganda Kiswahili ni moja wapo ya lugha zinazotumiwa katika maingiliano mengi ya kitaifa, vilevile kinafundishwa katika viwango mbalimbali vya shule za msingi na sekondari na hata katika baadhi ya vyuo vikuu nchini humo. Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kiswahili kinachukuliwa kama lugha ya ukanda, na mnamo mwaka 2016, bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki liliidhinisha Kiswahili kuwa lugha rasmi (Kakama, 2019: 1). Aidha, Kiswahili ni lugha rasmi ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuanzia Agosti 2019 (Kakama, 2019: 15). Kwa sasa Kiswahili kimevuka mipaka ya Bara la Afrika na kinafundishwa katika vyuo mbalimbali katika mataifa ya kigeni kama vile Ujerumani, Uingereza, Marekani, Urusi, Ufini, Ufaransa, Italia, Korea Kusini, Uchina, Oman na kadhalika (Whiteley 1969; Polome 1967; Chiraghdin na Mnyampala 1977; Massamba 2008; Chimerah 1998; Ripoti ya Kakama 2019; Niyomugabo 2019).

Burundi ni miongoni mwa baadhi ya nchi za Afrika ambako Kiswahili kimeenea kutokana na sababu kadha wa kadha. Vilevile, serikali ya Burundi inatambua lugha hiyo (tazama sera ya lugha ya Burundi ya mwaka 2014). Mpaka leo hii, Kiswahili kinafundishwa kama somo kuanzia shule ya msingi mpaka vyuo vikuu, vilevile kuna shahada ya awali na shahada ya umahiri wa Kiswahili. Aidha, lugha hiyo inatumika katika vyombo vya habari vya serikali na hata vya kibinafsi. Katika shughuli za kidini, kibiashara na usafiri lugha hii inatumika sana. Pia, vipo vyama mbalimbali ambavyo vinajihusisha na kuendeleza lugha hiyo nchini Burundi. Vyama hivyo ni kama SAPROS (Solution Academique à la Promotion du Swahili au Burundi), CHAWAKIBU (Chama cha Wanafunzi wa Kiswahili Vyuo Vikuu Burundi), CHAWAKIVIBU (Chama cha Walimu wa Kiswahili Vyuo Vikuu Burundi na kadhalika, vilevile ipo taasisi ya Kiswahili TAKUKIBU (Taasisi ya Kukuza Kiswahili Burundi).

Licha ya umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika maendeleo ya Burundi na ukanda wa Afrika Mashariki, bado kuna uhaba wa tafiti zinazoangazia sababu zilizopelekea kuenea kwa Kiswahili nchini humo na changamoto zinazotatiza maendeleo yake. Kwa mujibu wa Nshimirimana (2022), « lugha ya Kiswahili nchini Burundi inaendelea kushamiri hivi sasa ijapokuwa, kwa kulinganisha na umri wake nchini humo, wanazuoni wanaona kuwa ukuaji wake umekuwa wa taratibu sana ». Hali hii imechochea malengo ya utafiti wetu. Aidha, utafiti huu ni muhimu kwa sababu Burundi ni moja kati ya nchi za Afrika Mashariki. Wenyeji wake wanapaswa kuijua lugha ya Kiswahili na kuitumia

kwa mujibu wa itifaki iliyounda Jumuiya ya Afrika Mashariki (rejelea malengo ya Kakama). Ili kuweza kushughulikia maendeleo ya Kiswahili kama ilivyo katika mataifa mengine ya Afrika Mashariki, taifa la Burundi pia linapaswa kuunda baraza la Kiswahili. Ndiyo maana tafiti nyingi haswa zihusuzo maendeleo ya Kiswahili katika taifa hilo zinapaswa kufanyika ili kutoa mapendekezo kwa serikali na hatimaye kuongeza juhudi zake katika kukuza lugha hiyo na kukabiliana na tatizo la uhaba wa wataalamu wa Kiswahili.

Kwa hivyo, hali ya uhaba wa wataalamu na tafiti katika taaluma za Kiswahili nchini Burundi ilitusukumua kujiuliza maswali kadhaa. Je, taifa la Burundi linafanya vya kutosha kuendeleza Kiswahili? Kama Kiswahili kilipata kuingia Burundi, kiliingiaje? Ni kwa nini mwamko wa kusoma shahada za Kiswahili umeshika kasi sana miaka ya hivi karibuni katika taifa hilo (Kakama, 2019 :50)? Ni zipi changamoto zinazotatiza maendeleo ya lugha ya Kiswahili nchini Burundi? Je ni upi mustakabali wa lugha hii katika taifa hili? Haya ni baadhi ya maswali tuliyojitosa kujibu katika utafiti huu. Kutokana na mawanda na mipaka ya makala hii, utafiti huu ulijikita katika kujadili uenezaji na changamoto za Kiswahili nchini Burundi.

2. Nadharia ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Utabia iliyoasisiwa na Burrhus Frederic Skinner (1957). Utabia ni nadharia inayohusu tabia za wanyama na binadamu (Rutagwerela, 2020). Nadharia hii hueleza tabia bila kuhusisha matukio ya kiakili na michakato ya ndani kwenye ubongo bali huelezwa kwa kuhusishwa na sababu za nje za kimazingira. Kwa mujibu wa nadharia hii, inajadiliwa kuwa kurudiarudia ni muhimu katika kujifunza jambo (Bichwa, 2021). Aidha, wanautabia walidai kuwa katika kujifunza mchakato wa kiakili hauhusishwi. Wanaona kuwa kujifunza ni tokeo la uhusisho wa matukio, mwitiko wa kichocheo katika mazingira na uimarisho chanya au uimarisho hasi (Bichwa & Mwendamseke, 2021). Uimarisho chanya huhamasisha mwendelezo wa mwitiko, wakati uimarisho hasi hufifisha au kuzuia mwitikio usiendeleo. Katika nadharia hii fikra, hisia na dhamira si lazima kuhusishwa katika tabia za binadamu kama ilivyo kwa tabia za wanyama, iliyoonekana kama seti ya mwitikio katika vichocheo vya nje.

Katika nadharia hii, tafiti zinaeleza kuwa ujifunzaji wowote ukiwemo ujifunzaji wa lugha ulionekana kama uamiliaji wa tabia mpya. Nadharia hii inatambua nafasi ya mazingira katika uamiliaji na ujifunzaji wa lugha ya pili. Hapa izingatiwe kuwa mazingira yanatumika kwa maana pana zaidi kwa kuhusisha masuala ya utamaduni wa jamii ambayo hutumia lugha hiyo. Ujifunzaji wa lugha ni sawa na ujifunzaji mwingine wowote kutokana na kuiga modeli katika ingizo, kufanya mazoezi ya hiyo tabia mpya, na kutoa mrejesho sahihi. Bichwa (2021) anaunga mkono wazo la kwamba « mtu kujifunza lugha ni mwigo kwa maana ya kwamba anaiga kile kinachosemwa na watu wanaomzunguka. Anaendelea kudai kwamba « ujifunzaji wa lugha ni sawa na ujifunzaji wa tabia yoyote ile ya binadamu kama vile kuendesha baiskeli, kuogelea, na kadhalika.

Kwa mfano, anayejifunza jinsi watu wengine wanavyotamka sauti au maneno fulani naye anaiga na kufanya mazoezi ya utamkaji kutoka kwa wasemaji wazawa na hatimaye anaweza kutamka kwa usahihi. Kulingana na nadharia hii, uimarisho chanya na ingizo sahihi na ukosoaji wa kile ambacho si sahihi huwezesha mchakato wa ujifunzaji kufanikiwa. Nadharia ya Utabia inafaa kuhimili utafiti wetu kwa sababu ujifunzaji wa Kiswahili nchini Burundi umefanyika, kwa sehemu kubwa sana, kwa kuiga lugha hiyo kutoka, kwanza kwa Waarabu, na pili kutoka kwa jamii za Waswahili zinazozunguka nchi hiyo. Inaonekana kuwa, Warundi wengi wameipata lugha ya Kiswahili, siyo kwa kusoma darasani bali kwa kujenga tabia ya kuiga lugha hiyo. Kwa kuwa katika kuiga tabia mpya kunajitokeza dosari kadhaa, itakuwa sababu ya dosari zinazoshuhudiwa kwa wanafunzi wa Kiswahili vyuo vikuu nchini Burundi (tazama Butoyi & Elisifa, 2022). Aidha, watoto nchini Burundi hujifunza Kiswahili katika mazingira ya nyumbani na kukitumia kwa namna isiyo rasmi (Kakama, 2019: 46). Kwa mantiki hiyo, nadharia hii ilifaa kutuongoza katika kujadili sababu zilizopelekea kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini Burundi na changamoto zinazoikabili.

3. Mbinu za utafiti

Utafiti huu ulitumia data za uwandani na data za marejeleo. Kwa mujibu wa Kothari (2004), data za kwanza ni zile data ambazo hukusanywa kwa mara ya kwanza; yaani, data za uwandani.

Data hizo za awali za utafiti huu zilikusanywa kutoka kwa makundi kadhaa ya watafitiwa:

Kundi la Watafitiwa	Wanaume	Wanawake	Jumla
Walimu wa Kiswahili vyuo vikuu	4	4	8
Wakazi wa jiji la Bujumbura	7	8	15
Wakazi wa mkoa wa Rumonge	3	3	6
Wakazi wa mkoa wa Muyinga	3	3	6
Wakazi wa mkoa wa Makamba	3	3	6
			41

Aidha, walimu wa Kiswahili waliteuliwa kushiriki katika utafiti huu kwa sababu ndio wanaohusika pakubwa na kukuza Kiswahili nchini Burundi. Ifahamike kwamba wakazi wa mikoa ya Rumonge, Muyinga, Makamba na jiji la Bujumbura walishiriki katika utafiti huu kwa sababu mikoa hiyo inaongoza katika matumizi ya Kiswahili nchini Burundi. Katika kukusanya data, mtafiti alitumia mbinu ya usaili. Mbinu hii ni faafu zaidi kwa sababu inasaidia kupata data nyingi na za uhakika zaidi kuliko mbinu ya dodoso, vilevile inafaa kukusanya data kwa njia ya mtandao. Kwa mujibu wa Babbie (1992), usaili unahusisha mawasiliano ya moja kwa moja baina ya mtafiti na wahojiwa, na mtafiti hupata maelezo zaidi kuhusu baadhi ya mambo ambayo yasingeweza kuwekwa bayana kupitia mbinu nyingine ya utafiti. Aidha, mbinu hii ni njia inayotumika sana katika utafiti unaotumia mkabala wa kimaalezo kama ilivyo kwenye utafiti huu ambapo mtafitiwa alipewa nafasi ya kutoa maelezo kuhusiana na swali husika.

Mbali na hayo, utafiti huu ulitumia data za marejeleo. Data za marejeleo ni zile ambazo zimeshakusanywa, zimeshatumika na zimehifadhiwa (Kothari, 2004). Katika utafiti huu, mtafiti alikusanya data hizo katika makala na machapisho mbalimbali yenye uhusiano na utafiti huu. Pia, masuala ya maadili ya utafiti yalizingatiwa katika utafiti huu. Adam (2008) anaeleza kuwa, maadili ya utafiti ni pamoja na haki ya kuwa na usiri katika mchakato wa kupata data. Utafiti huu ulizingatia maadili yafuatayo: haki ya mtafitiwa kuhakikishiwa usalama wake; haki ya kujua madhumuni ya utafiti; haki ya kupata matokeo ya utafiti; haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti; na haki ya kujibu swali atakalopenda kujibu. Kijumla utafiti huu ulizingatia miiko yote ya maadili ya utafiti, ikiwa ni pamoja na kupata ridhaa ya watafitiwa. Aidha, uchanganuzi wa data za utafiti huu ulitumia mbinu ya mkabala wa kimaalezo. Kwa mujibu wa Enon (1998) mkabala wa kimaalezo ni mbinu ya kuchanganua data ambazo mtafiti hueleza na kufafanua data zake kwa kutumia maelezo.

4. Matokeo ya utafiti

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya utafiti huu kwa kutumia mkabala wa kimaalezo. Aidha, taarifa zilizokusanywa zinachambuliwa kwa kuanza na sababu zilizopelekea kuenea kwa Kiswahili nchini Burundi kisha changamoto zinazokabili uenezi huo.

1. Uenezaji wa Lugha ya Kiswahili Nchini Burundi

Sehemu hii inaangazia njia mbalimbali zilizopelekea kusambaa kwa lugha ya Kiswahili nchini Burundi. Nyenzo zinazojadiliwa katika sehemu hii ni: dini, uhamiaji, biashara, vita, maingiliano ya mpakani, ukoloni, ujio wa Waarabu, ushirikiano wa kikanda, elimu na ndoa.

a. Dini

Kwa kipindi kirefu, dini zimekuwa na nafasi kubwa katika kuendeleza lugha ya Kiswahili (Whiteley 1969; Mazrui na Mazrui 1995). Dini ambayo imechangia pakubwa kukua kwa Kiswahili ni dini ya Kiislamu; pamoja na hayo, dini ya Kikristo pia imekuwa na mchango usiopingika katika jukumu hilo. Kuanzia miaka ya 1970, Warundi waliohamia mataifa jirani walijiunga na makanisa na misikiti katika mataifa hayo ya Afrika Mashariki. Huko ugenini, katika masuala ya kuabudu, walikuwa wakitumia Kiswahili katika misikiti na makanisa hayo. Hata katika kambi nyingi za wakimbizi, ibada zilikuwa zikiendeshwa kwa Kirundi pamoja na Kiswahili. Taarifa zilizokusanywa kutoka kwa watafitiwa zinaonyesha kuwa mwaka wa 1972 ambapo taifa la Burundi lilikuwa limetumbukia kwenye machafuko ya kivita, Warundi wengi waliokuwa wamekimbilia katika mataifa jirani kama vile: Tanzania na Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, walikuwa na makanisa yao ambayo yalikuwa

yakiwaunganisha na wenyeji wa mataifa hayo, hivyo lugha ya Kirundi na Kiswahili zilikuwa zikitumika katika kuendesha shughuli za kidini. Matokeo yake, wakimbizi hao waliporejea nchini walikiendeleza Kiswahili kupitia huduma mbalimbali za kidini kama vile mahubiri, nyimbo na kadhalika. Mpaka leo, lugha ya Kiswahili inaonekana kutumika sana katika shughuli za kidini haswa, kwa Waislamu na Waprotestanti.

b. Uhamiaji

Uhamiaji umekuwa chanzo kikubwa cha kusambaza lugha (Blanchet, 2022). Burundi ni taifa ambalo linapakana na mataifa kadhaa yanayotumia Kiswahili, kama vile Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Ni dhahiri kwamba eneo la kijiografia la Burundi limechangia pakubwa katika kueneza lugha ya Kiswahili nchini humo. Mtu hawezi kuuliza kama Wakongo, Wakenya ama Watanzania wanakuja nchini Burundi kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama vile biashara. Mfano mzuri ni idadi kubwa ya Wakongo wanaopatikana jijini Bujumbura na hata katika mkoa wa Rumonge ambao wanajihusisha na shughuli mbalimbali kama vile biashara, elimu na kadhalika. Vilevile, Warundi wanaonekana kuhamia mataifa hayo jirani wakiwa na malengo tofautitofauti. Taarifa kutoka kwa watafitiwa zilionyesha kuwa kuna idadi kubwa ya Warundi ambao wapo nchini Kenya, Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Uwepo wao katika mataifa hayo umechangia pakubwa katika kukuza lugha ya Kiswahili nchini Burundi kwa sababu wanaporejea nchini wengi huendelea kutumia lugha hiyo. Data za utafiti huu zilionyesha kuwa Warundi wengi wamejifunza lugha ya Kiswahili katika mataifa jirani kama vile Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya na Tanzania. Aidha, uhamiaji unaendelea kuwa chanzo muhimu cha usambazaji wa Kiswahili kwa kuwa lugha inayounganisha eneo la ukanda wa Maziwa Makuu ni Kiswahili (Kakama, 2019), hivyo wahamiaji katika eneo hilo wanapendelea kutumia lugha hiyo.

c. Ujio wa Waarabu

Waarabu walipata kufika katika upwa wa Afrika Mashariki kuanzia karne ya nane na kuendelea. Mbali na malengo mengine, walikuja na lengo haswa la kueneza dini ya Kiislamu (Mazunya, 2011). Walipofika pwani ya Afrika Mashariki, iliwapasa kujifunza Kiswahili ili wakitumie kufanya mawaidha. Hivyo, kwa kufanya hivyo Kiswahili kilipata nafasi ya kutumika katika kueneza dini ya Kiislamu. Katika shughuli hizi za kidini Kiswahili kilitumika hadi bara ya Afrika Mashariki, mfano wa mikoa ya Kigoma na Tabora nchini Tanzania. Waarabu hawakuishia tu Tabora na Kigoma; walivuka mpaka nchini Burundi ambapo waliingia kupitia mwambao wa Ziwa Tanganyika (Mazunya, 2011; Chretien, 2005). Walipofika nchini Burundi, walianzisha vituo vya kufanyia biashara na kufundishia dini yao katika wilaya za Nyanza-lac, Rumonge na haswa jijini Bujumbura, vilevile katika mikoa ya Muyinga, Gitega na Cibitoke. Na hatimaye, watu hao waliweza kusambaa katika mikoa mbalimbali nchini Burundi, na maeneo mengi waliyoyakalia yaliitwa Uswahilini kwa kuwa lugha ya Kiswahili ndiyo ilikuwa ikitumika katika maeneo hayo. Kwa mujibu wa Gahama (1994: 485), Waarabu na Waswahili waliingia Burundi kutoka Ujiji, na kuanzisha vituo mbalimbali kama vile Magara, Rumonge na Kigwena. Mpaka leo hii, Waarabu wapo nchini Burundi na lugha wanayoitumia ni Kiswahili. Hivyo, kama ilivyo katika ukanda mzima wa Maziwa Makuu, Waarabu ndio wanaonekana kuwa chanzo kikuu cha kusambaa kwa lugha ya Kiswahili.

Maeneo haya yote ya Afrika Mashariki yalifikwa na Waarabu. Huko kote walitumia Kiswahili katika shughuli zao za kidini, kiutawala na kibiashara. Hapa Kiswahili kilipata kuenea. Hivyo, ujio wa Waarabu ulisaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Burundi.

d. Ukoloni

Mbali na data zinazonyesha kuwa lugha ya Kiswahili ilianza kushamiri nchini Burundi kuanzia karne ya nane, tafiti zingine zinadai kuwa lugha ya Kiswahili ilianza kuenea nchini Burundi mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Kwa mujibu wa Cazenave na Piarrot (2012: 2) akinukuliwa na Ntiranyibagira (2017: 2), "Kiswahili kililetwa Burundi na wafanyabiashara kutoka Tanzania mwishoni mwa karne ya kumi na tisa, mnamo mwaka wa 1897, na hivyo kuwa lugha ya kwanza ya kigeni kuzungumzwa nchini Burundi." Naye Bizongwako (2019: 37) na Ntahombaye (2005:46) wanadai kuwa, kabla ya ujio wa wageni, Kirundi ilikuwa lugha pekee iliyokuwa ikizungumzwa

nchini Burundi. Mtafiti huyo anaongeza kuwa Waarabu ndio walieneza lugha ya Kiswahili Burundi. Aidha, Kandagor (2018: 87) anadai kuwa

Kabla ya kuja kwa wageni katika pwani ya Afrika Mashariki, wenyeji walitumia Kiswahili kama lingua franca. Kwa jinsi hiyo, waliweza kumudu shughuli zao za kibiashara, kueneza dini na shughuli za kiutawala. Wageni walipowasili baadaye, walilazimika kujifunza Kiswahili ili waweze kukabilia na shughuli zao za kikoloni kikamilifu. Ukaloni uliposhamiri, shughuli za kukisanifisha Kiswahili zilianza katika mwaka wa 1925.

Mbali na ujio wa Waarabu, ongezeko la wimbi la lugha ya Kiswahili nchini Burundi linaweza kukadiriwa mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa kwa kurejelea kipindi ambapo ukoloni ulipoanza, haswa enzi za Wamisionari. Data zinaonyesha kuwa mwaka 1885 ndipo Wajerumani waliingia Burundi. Na Gahama (1994: 489) anadokeza kuwa Waarabu walikuwepo Burundi miaka ya 1860. Wengi wa Wajerumani hawa walikuwa wametoka Tanganyika ambapo walikuwa wamejifunza lugha ya Kiswahili (Chretien, 2005). Waliandamana na watumishi wao kutoka Tanganyika waliowasaidia katika shughuli za utawala. Ikumbukwe kuwa watumishi hawa walikuwa wazungumzaji weledi wa lugha ya Kiswahili. Waliozungumza lugha hii walionekana kuwa wangwana na wastaarabu. Baadae, walijenga misikiti katika baadhi ya vituo vyao ili kufunza dini ya Kiislamu. Eneo la Bujumbura lilitumika kama kitovu cha Waswahili nchini Burundi. Mafunzo yalitolewa kwa lugha ya Kiarabu na kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ambayo ilionekana kuwa nyepesi kwa wakazi wa maeneo haya. Wakoloni wa Kijerumani waliongeza jitihada katika kuendeleza Kiswahili ili kufanikisha mawasiliano baina yao na wakazi wa Burundi. Ikumbukwe kwamba hawakufanya hivi ili kumfaidi Mrundi kwa vyovyote vile, lakini nia yao ilikuwa kujiimarisha ili waweze kuendelea kuwakalia wenyeji kibeberu (Gahama 1994: 489).

Baada ya Mjerumani kushindwa katika vita vya kwanza vya dunia (1914-1918), mamlaka ya utawala wa eneo hili yalichukuliwa na Ubelgiji. Wabelgiji walieneza dini ya Kikristo, mfumo ambao ulikinzana na dini ya Waswahili iliyokuwa Uislamu. Wakoloni wa Kibelgiji walijaribu kwa kila njia kupinga lugha ya Kiswahili pamoja na dini ya Kiislamu. Kwa wakati mmoja Waswahili walifungiwa katika mji wa Usumbura. Lengo lao lilikuwa kuipa nguvu lugha ya Kifaransa. Bizongwako (2019: 38) anaeleza kwamba lugha ya Kifaransa ililetwa na wakoloni wa Kibelgiji mwaka 1916, kipindi ambapo Burundi ilianza kutawaliwa na Ubelgiji.

e. Ushirikiano wa Kikanda

Harakati za Jumuiya ya Afrika Mashariki bila shaka zitakuwa na athari kubwa katika maendeleo ya Kiswahili nchini Burundi. Ukweli ni kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Kakama, 2019: 19). Vilevile, kutakuwa na maingiliano makubwa miongoni mwa watu wa mataifa ya Jumuiya hiyo. Kiango (2022: 191), anaeleza kuwa katika miaka ya hivi karibuni, hususani baada ya kuanzishwa kwa sera za masoko huria, hali ya Afrika Mashariki imebadilika sana. Watu kutoka mataifa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki tayari wanasafiri hadi Burundi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi hususani biashara na hata elimu. Watu wa Burundi nao pia wanasafiri kwenda katika nchi mbalimbali za Jumuiya hiyo kwa ajili ya elimu na shughuli zingine. Kiango (2002: 191) anadokeza kwamba maingiliano haya ambayo yatashika kasi jinsi ushirikiano mpya wa Afrika Mashariki utakavyokuwa unaendelea kukua na kutekelezwa, yataanza kuibua suala la lugha ya kutumika katika kuwaunganisha na kuwashirikisha watu wengi zaidi na wa viwango tofauti vya elimu.

Wapo Warundi ambao wanazuru mataifa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki haswa Tanzania, Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ili kutafuta vibarua. Aidha, wapo Warundi wanaokaa katika mataifa hayo kwa sababu ya kazi za kiserikali na kazi zingine kama vile wafanyakazi wa balozi za Burundi katika mataifa hayo, wafanyakazi wa mamlaka ya mapato ya Burundi (OBR) na tawi la kiwanda cha FOMI nchini Tanzania, wafanyakazi katika ofisi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, na kadhalika. Lugha wanayoitumia kwa kiwango kikubwa, hasa katika mitagusano ya moja kwa moja na wenyeji wa mataifa hayo ni Kiswahili. Hali hii inaendelea kueneza lugha ya Kiswahili katika taifa la Burundi. Pia, maingiliano hayo yanarahisishwa na ushirikiano uliopo baina ya mataifa ya ukanda huo. Ushirikiano huo uliyafanya mataifa wanachama kuondoa vikwazo vya kusafiri kwa wenyeji wa Jumuiya hiyo, jambo ambalo limekuwa na athari chanya kwenye uenezaji wa lugha ya Kiswahili nchini Burundi.

f. Vita

Moja kati ya nyenzo kubwa zilizosaidia kuingia na kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini Burundi ni vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyoshuhudiwa miaka ya 1972 (Lemarchand, 2002:19), 1986, 1993 na mzozo wa kisiasa ulioikumba nchi hiyo mwaka 2015. Machafuko haya yalisababisha raia wengi wa Burundi kuhamia katika mataifa jirani kama vile Kenya, Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda, na Uganda ili kutafuta hifadhi. Mataifa haya ya Afrika Mashariki na eneo la Maziwa Makuu kwa kawaida yanazungumza lugha ya Kiswahili kama lugha ya maenezi mapana (Habwe, 2021: 62; akiwanukuu Chimerah, 1998; Mazrui na Mazrui, 1995). Wakimbizi hao walilazimika kukaa na kutagusana na wenyeji ambao waliwasiliana nao kwa kutumia Kiswahili.

Kwa mfano, mwaka 2009 serikali ya Tanzania iliwapa uraia wakimbizi toka Burundi walioingia nchini humo mwaka 1972 katika makambi ya wakimbizi ya Katumba, Mishamo na Ulyankulu. Baadae, mnamo mwaka 2015, kambi zingine: Nyarugusu, Nduta na Mtendeli zilifunguliwa kupokea kwa mara nyingine wakimbizi kutoka Burundi. Katika kambi ya Nyarugusu ambayo kwa kawaida ni kambi ya wakimbizi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, wakimbizi hao wa Burundi wanalazimika kutumia lugha ya Kiswahili katika mitagusano na wenzao kutoka Kongo na wenyeji wa mkoa wa Kigoma. Shughuli za kidini, kibiashara na elimu kati ya jamii hizo zimechangia kwa kiasi kikubwa katika kupelekea jamii ya wahamiaji hao wa Burundi kutumia lugha ya Kiswahili.

Wakimbizi wa Burundi waliporejea nyumbani baada ya miaka kadhaa wakiwa huko uhamishoni, walirudi huku wakiwa wajuzi wa lugha ya Kiswahili ambayo waliendelea kuitumia nchini katika miktadha tofautitofauti. Kwa kurejelea historia ya Burundi, mikoa ambayo ilisajili idadi kubwa ya watu waliowahi kukimbilia nchini Tanzania, inaongoza katika kuwa na idadi kubwa ya wazungumzaji wa Kiswahili. Mikoa ya Makamba, Rutana, Ruyigi, Muinga, Karusi, licha ya kuwa inapakana na Tanzania, taarifa zinasema kwamba inaongoza kuwa na idadi kubwa ya wazungumzaji wa Kiswahili.

Aidha, vita vinavyoendelea mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa miongo kadhaa vimechangia katika kuendeleza Kiswahili nchini Burundi. Raia wengi kutoka Kongo waliomba hifadhi nchini Burundi. Miongoni mwao wapo wanaokaa jijini Bujumbura kwa ajili ya masomo na shughuli zingine. Hali hiyo huwafanya Waswahili hao kuchangamana na Warundi, hivyo kusambaza lugha ya Kiswahili.

g. Biashara

Tafiti zinaonyesha kuwa biashara ndiyo lengo kuu la ujio wa Waarabu katika pwani ya Afrika Mashariki (Gahama, 1994: 489). Waarabu walifanya biashara kwa kubadilishana bidhaa na wenyeji wa Afrika mashariki (Habwe, 2021). Bidhaa kubwa walizoleta Waarabu zilikuwa ni nguo, viungo vya chakula, shanga, silaha na urembo. Bidhaa walizohitaji kutoka kwa Waafrika ni pembe za ndovu, dhahabu, watumwa na ngozi za wanyama. Katika shughuli hizi za kibiashara Kiswahili kilitumika. Taarifa zinasema kuwa misamiati mingi iliongezeka katika lugha ya Kiswahili kutokana na uhitaji wa biashara. Hivyo Kiswahili kilikua kimsamiati. Ifahamike kuwa Waarabu walifanya biashara na jamii za ukanda wa Afrika Mashariki. Hivyo, iliwalazimu kuunda misafara ya kwenda na kurudi. Gahama (1994: 483) anaeleza kuwa Waarabu walifika Tabora, Kigoma, Burundi hadi mashariki mwa Kongo kutokea Zanzibar. Huko kote walitumia Kiswahili kama lugha ya mawasiliano. Kwa kufanya hivyo Kiswahili kilienea. Hivyo, biashara iliwezesha Kiswahili kukua na kuenea. Rejelea Ramani ya Afrika Mashariki kuonesha misafara ya kibiashara wakati wa biashara kati ya wabantu na Waarabu! Mzagao huu ulisaidia Kiswahili kukua na kuwezesha misafara ya watumwa kutoka bara wakielekea pwani.

Mpaka zama za sasa, biashara inaendelea kuwa sababu muhimu ya kusambaa kwa Kiswahili katika ukanda wa Maziwa Makuu. Kiango (2002: 191) anasema kwamba wananchi wa kawaida ambao ni wafanyabiashara ndio kiungo kikubwa kwa sasa baina ya wazalishaji na wanunuzi. Naye Choge (2020: 6) anadai, “shughuli za kiuchumi zimechukua nafasi muhimu katika kueneza Kiswahili kijiografia na kimatumizi kwa karne nyingi. Kama ilivyo kabla ya uhuru, Kiswahili bado ni lingua franca katika biashara za kisasa kama vile za kunadi bidhaa sokoni, fedha, uchukuzi na usafirishaji katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.” Nchini Burundi, kunaoneka idadi kubwa ya Waarabu, Watanzania na Wakongo ambao wanajihusisha na shughuli za kibiashara. Katika kufanikisha

shughuli zao, lugha wanayoitumia kwa kiasi kikubwa ni Kiswahili, hivyo lugha hiyo huendelea kusambaa nchini humo.

h. Elimu

Kuenezwa kwa dini ya Kiislamu kulifungamana na utoaji wa elimu ya dini. Madrasa vituo vya kufundishia enzi hizo zilianzishwa ili kutoa elimu hiyo kwa watoto na vijana wa kibantu. Lugha iliyotumika kutoa elimu hiyo ni Kiswahili. Data zinaonyesha kuwa misamiati kama kitabu, darasa, bakora, juzuu na kadhalika, iliingia katika lugha ya Kiswahili. Pia, hati za Kiarabu zilitumika kuandika lugha ya Kiswahili. Mfano utenzi wa Fumo Lyongo ulianza kwa kuandikwa kwa hati za Kiarabu. Hivyo Kiswahili kilipata kukua. Elimu hiyo haikutolewa katika maeneo ya pwani tu bali iliendelea kutolewa hadi bara ya Afrika Mashariki. Maeneo kama Ujiji, Kondo na Tabora madrasa zilifunguliwa ili kutoa elimu hiyo ya kidini. Waarabu hao hawakuishia Tanzania tu, walivuka hadi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Burundi (Mazunya, 2011), na mfumo huohuo wa kuanzisha madrasa uliendelezwa. Hivyo Kiswahili kilipata kuenea. Ni wazi kwamba elimu iliyotolewa na Waarabu kwa Wabantu ilisaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili. Baadhi ya watoto wa kibantu walipata mawaidha ya dini ya Kiislamu kwa lugha ya Kiswahili. Mpaka leo hii, lugha ya Kiswahili ndiyo inatumika kufundishia dini ya Kiislamu nchini Burundi.

Elimu pia imekuwa wakala muhimu katika kusambaza na kutangaza lugha ya Kiswahili katika taifa la Burundi, kulingana na maoni ya wahojiwa kuhusu suala hili. Kwa mfano, Warundi waliowahili kuhamia nchini Tanzania, haswa miaka ya 1972 na 1993, taarifa zinaonyesha kuwa walikuwa wakipata elimu ya msingi kwa lugha ya Kiswahili; yaani, kwa kuzingatia mitaala ya elimu ya Tanzania. Kwa mujibu wa Choge (2020:- 4), “licha ya suala la utaifa, utekelezaji wa sera za elimu umeeneza Kiswahili kijiografia na kimatumizi. Baada ya uhuru, Kiswahili kimekuwa sehemu ya masomo ndani na nje ya Afrika Mashariki katika viwango vyote vya elimu japo ufundishaji wake haujawa sawa katika nchi zote.” Hivyo, vijana wengi waliweza kujifunza na kujinoa katika lugha ya Kiswahili. Aidha, wapo Warundi ambao, miaka hiyo, walibahatika kusoma vyuo vikuu vya Tanzania na Kenya, na baadae wakaja kufundisha Kiswahili nchini Burundi. Miaka ya sasa, idadi ya Warundi wanaosoma Kiswahili ugenini inazidi kuongezeka kutokana na ushirikiano wa kikanda (rejelea malengo ya Kakama).

Vilevile, Kiswahili kinafundishwa kwa sasa nchini Burundi kuanzia elimu ya msingi mpaka vyuo vikuu. Kama ilivyo, kuna elimu rasmi na elimu isiyo rasmi (M’Ngaruthi, 2021). Maana yake, Warundi wamejifunza lugha ya Kiswahili kupitia elimu rasmi; yaani, kupitia shule za serikali na taasisi nyinginezo, na elimu isiyo rasmi; yaani, kupitia vyama vya Kiswahili na utangamano na watu wa mataifa ya ukanda.

i. Ndoa

Mbali na masuala ya biashara na dini, Waarabu walioana na wakazi wa Afrika mashariki na kujenga makazi katika pwani na hata kwenye ukanda wa Afrika mashariki. Muunganiko huo wa kifamilia ulichochea uenezaji wa lugha ya Kiswahili kwa kuwa familia zilizotangamana na Waarabu hao ziliona haja ya kujifunza Kiswahili. Wahojiwa katika utafiti huu walithibitisha kwamba kadri Waarabu walivyosambaa ndivyo ndoa kati yao na Wabantu zilivyoongezeka na ndivyo lugha ya Kiswahili ilivyopata nafasi ya kuzungumzwa zaidi na zaidi. Taarifa zinaonyesha kuwa mji wa Rumonge nchini Burundi ulianzishwa na Waarabu miaka ya 1980. Ndoa kati yao na Warundi, na hata Wakongo na Warundi ni miongoni mwa sababu zilizopelekea mji huo kuwa na Waswahili wengi zaidi. Hivyo, ndoa kati ya Waarabu na Wabantu zilipelekea kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Burundi.

Kakika mkoa wa Rumonge na jiji la Bujumbura, kunaonekana Warundi ambao lugha yao mama ni Kiswahili (rejelea mtaa wa Buyenzi). Ilibainika kuwa wapo raia wengi kutoka Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo walioa nchini Burundi, na hivyo kufanya matumizi ya Kiswahili kuongezeka. Ukweli ni kwamba zipo hata shule jijini Bujumbura na mkoani Rumonge ambazo ni kwa ajili ya raia wa Kongo, na lugha inayotawala katika shule hizo ni Kiswahili.

Vilevile, raia wa Burundi waliohamia katika mataifa jirani na kukaa kwa muda mrefu walioa wachumba kutoka Burundi. Lakini kuna baadhi yao ambao walioa wachumba wa huko ugenini. Matokeo yake, licha ya kuendeleza lugha ya Kiswahili, baadhi waliamua kurejea nchini na familia

zao na wengine waliendelea kubaki uhamishoni. Katika kukusanya taarifa za utafiti huu, kuna mifano kadhaa iliyotolewa ya Warundi waliooa ama kuolewa ugenini haswa nchini Tanzania, Kenya, Uganda na hata Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Aidha, watoto waliozaliwa katika mazingira hayo walipelekwa katika shule za huko ugenini, hivyo wakapata nafasi ya kujiimarisha zaidi katika lugha ya Kiswahili na hatimaye kusambaza maarifa hayo wanaporejea nchini.

j. Maingiliano ya Mpakani

Nchi ya Burundi, kama ilivyoelezwa hapo awali, inapakana na nchi ya Tanzania, Rwanda, vilevile nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Kwa muda mrefu kumekuwa na maingiliano ya mipakani ambayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kuisambaza lugha ya Kiswahili katika mataifa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Kakama, 2019: 38). Katika kukusanya taarifa za utafiti huu, mpaka wa Katumba ulitolewa kama mfano mzuri kuonyesha namna raia kutoka pande mbili; yaani, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, wanavyochangamana katika eneo hilo la Katumba na kulifanya kuwa na wazungumzaji wengi wa Kiswahili. Maeneo mengine ya mpakani kama vile: Kobero, Mugina, Rumonge yalitajwa kuwa na wazungumzaji wengi wa Kiswahili kutokana na shughuli mbalimbali katika mipaka hiyo.

Ni dhahiri kuwa biashara za mipakani zimechangia pakubwa katika kukuza lugha ya Kiswahili katika mataifa ya Maziwa Makuu, haswa nchini Burundi ambapo jiji kuu la Bujumbura linapakana na jiji la Bukavu kwa upande wa Kongo, na hivyo kurahisisha uhamiaji na mzunguko wa biashara na uhamiaji kati ya mataifa hayo.

k. Vyombo vya Habari

Kakama (2019: 30) wanaeleza kuwa vyombo vya habari ni asasi muhimu sana katika kukuza na kueneza lugha yoyote ile, hasa katika enzi hizi za utandawazi. Taasisi hiyo inaongeza kwamba vyombo vya habari hujizatiti kutumia lugha teule inayoeleweka kwa hadhira lengwa. Naye Mwansoko (1995) anadai kuwa vyombo vya habari vina jukumu la kuwasilisha taarifa mbalimbali kwa hadhira mbalimbali kutegemeana na muktadha husika. Anasisitiza kuwa mafanikio ya vyombo vya habari katika kuufikisha ujumbe kwa usahihi kwa watu hutegemea sana uelewa mzuri wa istilahi zinazohusiana na mada anuwai wanazozishughulikia waandishi na watangazaji wa habari. Kwa upande mwingine anasisitiza kuwa ujuzi na ufahamu wa lugha ni kipengele muhimu katika uandaaji na usambazaji wa habari katika vyombo vya habari.

Kwa mantiki hiyo, ni dhahiri kuwa vyombo vya habari vimetoa mchango mkubwa katika kukuza na kuendeleza Kiswahili nchini Burundi. Kwa mujibu wa Kiango (2002: 194), "...ni kwamba vyombo vya habari vitasaidia kukisambaza Kiswahili kwa haraka na kukuza uwezo wa lugha wa watumiaji wake." Tangu miaka mingi iliyopita, vituo mbalimbali vya redio ikiwemo redio na televisheni ya taifa (RTNB) vimekuwa vikirusha vipindi na matangazo katika lugha ya Kiswahili. Kwa asilimia kubwa ya vituo vya redio vilivyosajiliwa nchini Burundi hutumia, miongoni mwa lugha zingine, lugha ya Kiswahili, katika kuendesha vipindi, kurusha matangazo na kutoa taarifa ya habari. Vituo vya redio kama: Radio Isanganiro, *RTNB, Radio Bonesha, Radio Scolaire Nderagakura, Radio Izere FM, nk. hutumia lugha mbalimbali ikiwemo lugha ya Kiswahili katika shughuli zake, vilevile mitandao ya kijamii haiwezi kuwekwa pembeni katika kuendeleza Kiswahili. Choge (2020: 11) anasema, "hivi sasa, wavuti na mitandao ya kijamii imeanza kuchukua nafasi muhimu katika uenezi wa Kiswahili."

Vilevile, vituo vya redio vimesaidia kuendeleza Kiswahili nchini Burundi kupitia nyimbo za burudani na za kidini, na hata kupitia vipindi mbalimbali vinavyowapa nafasi wadau wa Kiswahili kuzungumzia maendeleo ya lugha hiyo. Hapa tunaweza kutoa mfano wa Radio Scolaire Nderagakura, kituo cha redio ambacho ni maarufu sana katika kutetea lugha ya Kiswahili nchini Burundi.

5. Changamoto Zinazoikumba Lugha ya Kiswahili Nchini Burundi

Ni kweli kwamba lugha ya Kiswahili imeendelea na inazidi kushamiri nchini Burundi licha ya changamoto kadhaa zinazoikabili lugha hiyo. Sehemu hii inajadili matatizo mbalimbali yanayodhaniwa kutatiza uenezaji kwa haraka wa lugha ya Kiswahili nchini Burundi. Aidha, katika kukusanya data za utafiti huu, ilibainika kuwa Kiswahili kilichelewa kukua nchini Burundi

ikilinganishwa na mataifa jirani na eneo lake la kijiografia; yaani, hali ya kuwa Burundi ipo katikati mwa jamii zinazozungumza lugha hiyo ingekuwa chanzo cha kuwa na idadi kubwa zaidi ya wazungumzaji na haswa walimu wa kutosha wa Kiswahili. Kwa mujibu wa Nshimirimana (2022), mhadhiri wa Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Burundi tangu mwaka 1993, “lugha ya Kiswahili nchini Burundi inaendelea kushamiri hivi sasa ijapokuwa kwa kulinganisha na umri wake nchini humo, wanazuoni wanaona kuwa ukuaji wake umekuwa wa taratibu mno.” Katika kujadili changamoto hizo, tulijikita katika data za marejeleo na kwa kiasi kidogo, katika data za uwandani. Mwanazuoni Nshimirimana (2022) anataja changamoto za kihistoria zilizokwamisha ukuaji wa lugha ya Kiswahili nchini Burundi.

a. Upinzani kati ya wafanyabiashara wa Kiarabu na Wakoloni

Nshimirimana (2022) anataja mbinu ya wakoloni ambao hawakuwapokea vizuri wafanyabiashara wa Kiarabu na badala yake waliwatenga katika maeneo maalum ili Kiswahili kisienee. Anatoa mifano akisema Waarabu walipofika maeneo mathalani Bujumbura, waliwekwa Buyenzi. Wakipita njia ya Kigoma, Tanzania, basi waishie Rumonge nchini Burundi na wasisambae katika maeneo mengine nchini. Anaongeza kuwa hata leo mkifanya utafiti, kila mkoa kuna sehemu ambayo inaitwa uswahilini kwa sababu ya ujanja wa wakoloni.

Hata hivyo mwanazuoni huyo anaeleza kuwa lugha ni kama mafuriko makubwa ya maji, huwezi kuyazuia kwa mikono akitoa mfano kuwa, kwa kuwa Kiswahili kilitumika kama lugha ya harakati za ukombozi, kwenye redio za Afrika Mashariki sanasana kama Tanzania walikuwa wanaimba nyimbo za Kiswahili za kufukuza mkoloni. Wakati wanaimba hizo nyimbo zilikuwa zinakuja hata kwenye redio zetu za Burundi. Mwaka 1961 redio ya Burundi ilianza kutoa nyimbo za Kiswahili.

Upinzani huo kati ya Mwarabu na mkoloni ulijidhihirisha pia katika masuala ya dini ambapo wakoloni walilenga sana kuendeleza dini ya Ukristo na kuachana na dini ya Uislamu. Dini ya Uislamu ilieneza kwa lugha ya Kiswahili ilhali dini ya Ukristo ilisambazwa kwa Kifaransa. Kutokana na nguvu na ushawishi wa mkoloni, lugha ya Kifaransa ilianza kutawala dhidi ya Kiswahili.

b. Vita kati ya jeshi la Mfalme na Waarabu

Wakati Waarabu walipoingia nchini Burundi kupitia njia ya Ujiji, Kigoma Tanzania, wakipitia mwambao wa Ziwa Tanganyika na kabla ya kuingia ndani ya nchi ya Burundi wakaonwa na wenyeji ambao waliwashangaa na kwenda kutoa taarifa kwa Mfalme wa wakati huo kwamba, kwa namna walivyoonekana, Waarabu hao ni kama walikuwa wanakuja kuivamia Burundi. Mfalme akatoa amri ya kupambana nao. Kutokana na mapigano kati ya wanamgambo wenyeji na Waarabu waliojilhami kwa bunduki, uhasama huo ukakwamisha kupokelewa kwa mikono miwili Waarabu na maneno yao ya mchanganyiko wa Kiarabu na kibantu, na bila shaka ikawa kizuizi cha Kiarabu kuchanganyika zaidi na Kibantu cha Wabantu wa Burundi.

Nshimirimana (2022) anaeleza kuwa, “hata hivyo kutokana na mapigano hayo ambapo Waarabu walitumia maneno ya Kiswahili ya ‘piga maliza wote’ ndimo lilimozaliwa neno ‘Rumaliza’ lililoanza kutumika nchini Burundi kuitambua lugha ya Kiswahili kama lugha ya Rumaliza ; yaani, lugha ya kuwamaliza Warundi.”

c. Matumizi ya maneno kama vile “leta mayai”, “leta siagi”

Namna Waarabu walivyotumia maneno ya Kiswahili kuwalazimisha wenyeji kuleta mali zao kwa wakoloni, mathalani wenyeji walipoambiwa, “leta mayai, leta siagi...leta...ilionekana kwa Warundi kama lugha ya wezi na wanyanganyi. Hivyo, hali hiyo ilipelekea kuchukiwa kwa lugha ya Kiswahili na ikaonekana kuwa lugha ya kunyanganya Warundi, hivyo basi si lugha ya kusemwa. Kwa maana hiyo lugha ya Kiswahili ikaanza kupoteza mvuto kwa Warundi.

d. Ukatili wa Wakoloni

Ukatili wa wakoloni kwa Warundi ulichangia katika kupoteza thamani kwa lugha ya Kiswahili. Sababu ilikuwa ni namna wenyeji walivyokuwa wanapigwa viboko bila kujali rika wala hadhi yao katika jamii na kwa kawaida mtu akilazwa chini na kucharazwa viboko nane. Amri ilikuwa inasema ‘lalia nane’ ; yaani, lala chini ili upigwe viboko nane. Hapo ndipo wenyeji ; yaani, Warundi wakaona

hii lugha ya lalia nane, si lugha rafiki ya kusemwa. Izingatiwe kwamba mkoloni alitumia lugha ya Kiswahili ili aweze kudumisha utawala wake kwa sababu lugha hiyo ilikuwa imeshaendelezwa na Waarabu. Sasa, matumizi ya lugha hiyo katika kuwatawala Warundi kimabavu yakasababisha kususiwa kwa lugha ya Kiswahili nchini humo.

e. Imani potofu kuhusu Kiswahili

Changamoto nyingine ya kihistoria iliyotatiza maendeleo ya Kiswahili kwa kasi nchini Burundi ilikuwa ni imani potofu iliyojengwa na Warundi ambao ni wafugaji wa ng'ombe walipoamini kuwa mtu akizungumza lugha ya Kiswahili, na mdomo huohuo ulioyatamka maneno ya Kiswahili ukanywa maziwa ya ng'ombe, basi ng'ombe huo atakufa. Aidha, Warundi walijijengea imani kuwa kila anayezungumza lugha ya Kiswahili ni tapeli, hivyo lugha ya Kiswahili ikaonekana kuwa lugha ya matapeli, licha ya umuhimu wake. Kiango (2022 : 188) anadai kuwa « dhima kuu ya lugha yoyote ni kukidhi haja ya mawasiliano katika jamii yenye utamaduni mmoja. Pamoja na dhima hiyo muhimu, lugha hutumika pia kama kitambulisho cha jamii fulani, vilevile kama njia mojawapo ya kuelezea na kuhifadhi utamaduni wake ». Pia, zilikuwepo imani kwamba anayezungumza Kiswahili ni muislamu. Kwa wakatoliki ilikuwa mwiko kuzungumza lugha ya Kiswahili. Mambo hayo yalipelekea kuchelewa kwa Kiswahili kusambaa nchini Burundi.

f. Uhaba wa walimu na vitabu

Jambo jingine ambalo linaonekana kuwa kipingamizi kwa harakati za kuendeleza Kiswahili nchini Burundi ni uhaba wa walimu na vitabu (Kakama, 2019 : 47). Taarifa kutoka kwa wahojiwa zinaonyesha kuwa walimu wengi wanaofundisha shule za sekondari walifuzu mafunzo ya Kiswahili kupitia Sapro Burundi. Taarifa kutoka kwa walimu wa Kiswahili vyo vikiu nchini Burundi zinaonyesha kuwa mpaka mwishoni mwa mwaka 2017, vijana takribani 2000 walikuwa wamefuzu mafunzo ya Kiswahili kupitia Sapro Burundi.

Baadae, vyama vingine kama CHAWAKIBU vimejitosa na kutoa mafunzo ya Kiswahili. Changamoto kubwa ni kwamba mafunzo hayo siyo faafu kumuandaa mwalimu wa sekondari. Vilevile, vyo vikiu kunaonekana uhaba wa walimu. Na matokeo yake ni kuchelewa kwa wanafunzi wa shahada ya umahiri kuhitimu masomo kwa kuwa walimu wanapatikana kwa shida. Mara nyingi walimu wa kufundisha Kiswahili kwa ngazi ya umahiri hutoka nchini Tanzania na Kenya.

g. Sera ya lugha ya Burundi

Sera ya lugha ya Burundi ni changamoto nyingine katika juhudi za kuinusuru lugha ya Kiswahili (Irankeje, 2022: 234). Serikali ya Burundi inatambua lugha tatu rasmi ambazo ni Kirundi, Kifaransa na Kiingereza (Tazama sera ya lugha ya Burundi ya mwaka 2014). Lugha hizo zinaonekana kupewa nafasi kubwa sana katika shughuli mbalimbali na haswa katika sekta ya elimu. Lugha ya Kiswahili siyo miongoni mwa lugha rasmi za Burundi. Sababu hiyo hupelekea kupewa nafasi ndogo katika shughuli za kiserikali na hata katika ufundishaji. Kwa mujibu wa sera ya lugha ya Burundi ya mwaka 2014, lugha ya Kiswahili inafundishwa kuanzia shule ya msingi mpaka vyo vikiu. Licha ya kuanzishwa kwa shahada za Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Burundi na katika taasisi ya ualimu, ENS, bado lugha ya Kiswahili inapewa nafasi ndogo sana katika uwanja wa elimu. Masaa ya Kiswahili katika shule ya msingi ni machache sana ikilinganishwa na lugha zingine zilizobaki. Matokeo yake ni uhaba unaoshuhudiwa wa wataalamu na machapisho ya Kiswahili. Vilevile, kuna hatari ya kukwamisha juhudi za kuendeleza lugha hiyo kutokana na kukosa motisha ya kujifunza lugha hiyo kwa baadhi kisa haina maana kubwa katika jamii. Yaani, sera ya lugha ya nchi ndiyo chanzo cha maendeleo ya lugha husika katika taifa hilo (Kakama, 2019: 22).

Jedwali lifuatalo linaonyesha mpangilio wa masaa ya kufundisha lugha hizo kwa wiki shule za sekondari kuanzia darasa la 7 hadi la 9 pamoja na kidato cha lugha:

Somo	Masaa kwa Wiki	Ngazi ya Elimu
Kiswahili	1	Darasa la 7 hadi la 9
Kiingereza	5	
Kifaransa	5	
Kirundi	2	
Kiswahili	5	Kidato cha Lugha
Kiingereza	10	
Kifaransa	10	
Kirundi	4	

Aidha, licha ya kuwa lugha ya pili inayozungumzwa nchini Burundi (Mazunya : 2011), lugha ya Kiswahili inapewa nafasi finyu katika nyanja mbalimbali haswa katika uwanja wa utawala wa umma ambapo lugha zinazotumika ni Kirundi na kifaransa.

h. Matabaka ya kiuchumi

Historia ya Burundi iliathiri sana matumizi ya lugha ya Kiswahili. Nshimirimana (2022) anaeleza changamoto za kihistoria zilizodidimiza ukuaji kwa haraka wa Kiswahili nchini Burundi kutokana na mitazamo potofu iliyojengwa na Warundi dhidi ya lugha hiyo. Maneno kama yale: leta mayai, leta siagi, lalia nane, yalipelekea Warundi kuiona lugha ya Kiswahili kama lugha ya wanyang'anyi, hivyo siyo lugha ya kuongea (Nshimirimana, 2022). Mitazamo hiyo ilikuja kutiwa chumvi na matabaka ya kiuchumi na kikabila. Kwa mujibu wa Irankeje (2022: 234), tofauti za kikabila zimekuwa changamoto katika kuendeleza Kiswahili nchini Burundi.

Mitazamo hiyo iliendelea mpaka leo ambapo watu, haswa wa tabaka la juu, huiona lugha hiyo kama lugha ya mtaani na lugha ya matapeli. Vilevile, watu wa tabaka la chini huiona lugha ya Kiswahili kama lugha ya biashara (Benaou, 1982:28). Aidha, watu wa tabaka la juu wanahimiza watoto wao kuweka nguvu katika lugha za Ulaya kuliko lugha ya Kiswahili (Irankeje, 2022: 234). Maana yake, watoto kutoka familia zenye kipato cha juu huwa na ndoto ya kuzuru ama kuendelea na masomo ughaibuni ilhali mtoto wa maskini huchukulia lugha ya Kiswahili kama njia ya mafanikio yake atakapovuka kwenda kutimiza ndoto yake katika mataifa jirani ambayo kwa kawaida huzungumza lugha ya Kiswahili. Kiuhalisia, siyo rahisi kuona familia za tabaka la juu wakipambania kujifunza Kiswahili. Na kwa kurejelea mitaa ambamo Kiswahili kinazungumzwa sana itakuwa ngumu kupata idadi kubwa ya wazungumzaji wa Kiswahili katika mitaa ya watu wenye kipato cha juu.

6. Hitimisho

Kwa kuhitimisha, ni wazi kwamba lugha ya Kiswahili ipo nchini Burundi na inaendelea kukua kwa kasi licha ya changamoto za kihistoria zilizotatiza ukuaji wake. Aidha, ni wazi kwamba Kiswahili ni lugha hai nchini Burundi na mambo yaliyowezesha kusambaa kwa lugha hiyo kama : dini, uhamiaji, vita, ujio wa Waarabu, miingiliano ya mpakani, biashara, elimu, ushirikiano wa kikanda na vyombo vya habari yameelezwa. Japokuwa imani potofu kuhusu Kiswahili pamoja na idadi ndogo ya waliosomea lugha hiyo vinaendelea kuwa vipingamizi katika harakati za kuendeleza lugha hiyo, serikali ya Burundi, taasisi za kimataifa na wadau wengine wa Kiswahili wanaonekana kuongeza kasi katika kuinusuru lugha hiyo. Mwisho kabisa, utafiti wa kina unahitajika ili kutathmini hali ya sasa ya maendeleo ya Kiswahili nchini Burundi na hatimaye kuweza kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazokwamisha juhudi za kuendeleza lugha hiyo.

Marejeleo

1. Ababaker, E. A. (2013). Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili na Athari Zake kwa Jamii ya Kiarabu : Mtazamo wa Kilughawiyajamii. Tasnifu ya PhD. Kiswahili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
2. Babbie, E. (1992). *The Practice of social Research 6th Ed.*, California: Wadsworth Publishing Company.

3. Benaou, A. (1982). Recherches sur le swahili du Burundi : Les nominaux. PhD thesis, HAL, University of Nice.
4. Bichwa, S., & Mwendamseke, F. (2021). Ufaafu wa Matumizi ya Nadharia ya Utabia katika Mbinu za Kufundishia Lugha ya Kigeni. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *Kioo cha Lugha, Juz. 19(2), 2021, 92-102.*
5. Bizongwako, A. (2019). Évaluation du Programme de Formation d'interpretes de l'université de Ngozi au Burundi. Chuo Kikuu cha Buea, Cameroon.
6. Blanchet, P. (2022). Migrations, Langues, Intégrations : une Analyse Sociolinguistique Comparative sur des Stratégies étatiques et familiales. Université Rennes 2, Bretagne, France.
7. Butoyi, D., & Elisifa, Z. (2022). Dosari za Kisarufi za Wanafunzi Wanaojifunza Kiswahili Sanifu katika Vyuo Vikuu nchini Burundi. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *Kioo cha Lugha, Juz. 20 (2), 239-256.*
8. Chimera, R. (1998). *Kiswahili, Past Present and Future*. Nairobi: University of Nairobi.
9. Chiraghdin, S. & Mnyampala, M (1977). Historia ya Kiswahili. Nairobi: Oxford University Press.
10. Chretien, J. P. (2005). Les premiers voyageurs étrangers au Burundi et au Rwanda: les « compagnons obscurs » des « explorateurs ». Afrique d'Histoire.
11. Choge, S. C. (2020). Uenezi wa Kiswahili baada ya Uhuru wa Afrika Mashariki kwa Mtazamo wa Nadharia ya Mifumo Changamano. Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro. *Kioo cha Lugha 2020, 18: 1-21.*
12. Gahama, J. (1994). Les Zanzibarites et le Burundi, XIXe- XXe Siecle. Omaly Sy Anio.
13. Habwe, J. H. (2021). Maenezi ya Lugha ya Kiswahili Nchini Sudan Kusini: Mafanikio na Changamoto. *Swahili Forum 28 (2021): 58-71.*
14. Hakizimana, H. (2017). Taasisi ya Sapro yasema Kiswahili chashamiri Burundi. Taarifa ya habari 31 Agosti, 2017, VOA.
15. Fiacre, I., & Anitha, N. (2022). Negative impact of multiculturalism on the use of standard Kiswahili in Burundi. *Journal of African History, Culture and Arts, 2(4), 234-247.*
16. KAKAMA (2019). Capacity Assessment of the Development and Use of Kiswahili in the EAC. Zanzibar.
17. Kandagor, M. (2018). Juhudi za Vyombo vya Habari katika Kukuza na Kueneza kiswahili Nchini Kenya. *Kioo cha Lugha. Juz.10.*
18. Kiango, J. G. (2002). Nafasi ya Kiswahili katika Ujenzi wa Jamii Mpya ya Afrika Mashariki. University of Dar es Salaam, Tanzania. *Nordic Journal of African Studies 11(2): 185-197 (2002).*
19. Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. 2nd Edition, New Age International Publishers, New Delhi.
20. Lemarchand, R. (2002). Le genocide de 1972 au Burundi : les silences de l'histoire. Dialogue n° 228, May-June 2002.
21. Lianza, V. (2021). Le swahili gagne en popularité dans le monde. Education & Culture, UN.
22. Massamba, D. (2008). Historia ya Kiswahili. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
23. Mazrui, A. A., & Mazrui, A. (1995). *Swahili state and society: The political economy of an African language*. East African Publishers.
24. Mazunya, M. (2011). Les Défis Linguistiques au Sein de l'East African Community: cas de l'Identité Francophone du Burundi. Les Cahiers de l'Orient.
25. M'Ngaruthi (2021). Mchango wa Lugha za Kiasili katika Uafikiaji wa Maendeleo Endelevu. East African Scholars Publisher, Kenya.
26. Mwansoko, H. J. M. (1995). Dhima ya Kamusi katika Kusanifisha Lugha. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
27. Niyomugabo, C. (2019). *Kiswahili nchini Rwanda: ufunguo wa maendeleo endelevu*. Katika Ken Walibora et al. (Wah), Kiswahili, Utangamano na Mendeleo Endelevu Afrika Mashariki. Zanzibar: KAKAMA: 68-79.
28. Nshimirimana, D. (2022). Burundi na Kiswahili, hizi ni baadhi ya changamoto za kihistoria zilizotukwamisha. Habari za UN.
29. Ntahombaye, P. (2005). Ethnicité et Citoyenneté au Burundi. Université du Burundi.
30. Ntiranyibagira, C. (2017). La politique Linguistique du Burundi: Evolution et Perspectives. *Revue Sénégalaise de Langues et de Littérature, 10 (1), 69-80.*

31. Polome, E. (1967). *Swahili Handbook*. Washington D. C.: Centre for Applied Linguistics.
32. Rutagwerela, D. J. (2020). Nadharia za Awali katika Uamiliaji wa Lugha ya Pili. Mwanagenzi Chuo kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya taaluma za Kiswahili Idara ya lugha ya Kiswahili na Isimu.
33. Whiteley, W. (1969). *Swahili: The Rise of a National language*. Methuen & Co. LTD: London.



Copyright © 2023: by the author/s. This article is licensed and distributed under an [Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International \(CC BY-NC-SA 4.0\)](https://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/)